		<p>Sasa Kila mmoja: Hii ni herufi <b>aA</b>. (Onesha wanafunzi herufi <b>aA</b>.) Herufi <b>aA</b> inaunda sauti gani, kila mmoja? Nyoosha mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja na wewe. (Darasa zima) <b>/aaa/</b></p> <p><i>Sasa, kila mmoja: hii ni herufi <b>kK</b>. (Onesha wanafunzi <b>kK</b>.) Herufi <b>kK</b> inaunda sauti gani? Nyoosha mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja na wewe. (darasa zima) <b>/k/</b></i></p> <p><i>Sasa, kila mmoja: hii ni herufi <b>il</b>. (Onesha wanafunzi <b>il</b>.) Herufi <b>il</b> inaunda sauti gani? Nyoosha mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja na wewe. (darasa zima) <b>/i/</b></i></p>	
--	--	--	--

★ ★ **Mazoezi ya Sauti ya herufi na Ufasaha (Dakika 4-5): MAZOEZI**

- Chukua kadi zenye herufi **mM, aA, kK, il** (AU andika herufi hizo ubaoni).
- Wakumbushe wanafunzi jina la kila herufi kisha onesha moja baada ya nyingine huku ukiwataka wanyooshe mkono kama wanajua majina ya herufi hizo.

**(Tumia sekunde 30 au zinazokaribiana kwa zoezi hili)**

- Sema sauti ya herufi **mM**
- Waeleze wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kusema jina

la herufi linalounda sauti hiyo. Fanya hivyo kwa **aA, kK, il**

- Waulize wanafunzi kama wanaweza kusoma neno kwa kulitamka. Onesha neno; **[Kaa, Ima]** kwenye ubao na useme **“Tizama Maandishi”**.
- Waoneshe namna ya kutamka neno (**Ninatenda, Tunatenda, Unatenda**) /k/ /a/ /a/.
- Unganisha sauti kisha sema neno **[kaa, ima]**.
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kusema sauti zilizomo katika neno **[kaa, ima]**, kisha watamke neno lote
- Chagua wanafunzi kadhaa kutamka neno hilo.
- Sahihisha makosa.
- Onesha neno kisha tamka sauti zinazounda neno
- Onesha neno kisha waambie wanafunzi walitamke. **[Mnatenda]**.
- Onesha kila herufi kasha tamka pamoja na wanafunzi. auti ya mwanzo katika neno **[kaa]** ni /k/, inayofuata /aaa/, ya mwisho /aaa/. Ni neno gani hilo? **[kaa]**. Neno ni **[mama]**.
- Sasa zamu yenu. Neno gani? **[kaa]**
- Waambie wanafunzi waandike herufi mpya, silabi na maneno ambayo yamefundishwa katika kipindi hicho (**Ninatenda, Tunatenda, Unatenda**)

### **Mchezo wa kujenga ufasaha** kutumia maneno **[Kaa, Kama, Kima, Ita, Mama, Maka]**

- Waeleze wanafunzi wanyooshe mkono wanpoona neno wanalolitambua katika kadi utakayoonyesha (au onesha maneno hayo ubaoni).
- Waambie kuwa utaonesha kila kadi (au utaonesha ubaoni) kwa haraka, kwa hiyo waharakishe kunyoosha mkono pindi wanapoona neno wanalolitambua
- Chagua mwanafunzi aliyenyoosha mkono asome neno husika.

### **Msamiati: (Dakika 4-5)**

Rudia maneno **[mama]**

### **Ufahamu wa Kusikiliza** (Dakika 10):

Wasomee hadithi ifuatayo. **ANGALIZO:** Msamiati na maneno rejea yamekozeshwa na yamepigwiwa mstari. Yaandike maneno ubaoni. Unapofikia msamiati wakati wa Mwanafunzi aweze kujibu maswali ya ufahamu, tulia kwa muda kisha onesha msamiati huo ubaoni.

## Hadithi ya Kusoma kwa Sauti [Hadithi kutoka kwenye kitabu]

- Andika hadithi kutoka kwenye kitabu ubaoni.
- Andika jina la mwandishi wa hadithi ubaoni
- Andika jina la msanifu wa michoro ubaoni.

### Rejea neno la hakiba:

- Andika neno [**mama**] ubaoni.
- Wakumbushe wanafunzi kuwa neno hili limekwisha fundishwa. Waambie walitumie katika sentensi kwa usahihi

## 11.0 Kufundisha sauti s

### Wiki ya 3: Siku ya 1

<p>Tarehe: _____</p> <p><b>Muongozo wa ufundishaji:</b> Tumia <b>jina la herufi/sauti ya herufi</b> katika muongozo huu ili kufundisha majina na sauti za herufi husika</p> <p><b>Malengo:</b></p> <ul style="list-style-type: none"><li>• Mwanafunzi aweze kutamka sauti na jina la herufi sauti na jina la herufi <b>s</b> kwa kutumia muongozo ufuatao</li><li>• Mwanafunzi aweze kufanya mazoezi ya kusoma kwa kutumia kadi za herufi, maneno na sentensi</li><li>• Mwanafunzi aweze kusoma sentensi rahisi</li><li>• Mwanafunzi aweze kujibu maswali ya ufahamu</li></ul>	<p><b>Zana:</b></p> <ul style="list-style-type: none"><li>• Kadi za herufi <b>s</b></li><li>• Kadi za herufi kwa ajili ya marudio</li><li>• Kadi za maneno</li><li>• Andika neno [<b>saa</b>] ubaoni</li><li>• Kadi za sentensi</li><li>• Hadithi au Nyimbo</li><li>• Kitini cha mazoezi kwa mwanafunzi</li></ul>
--	---

### Muongozo wa kufundisha utambuzi wa sauti (Dakika 5)

#### Marudio:

- Rudia sauti zilizofundishwa katika wiki hiyo: /a/, /m/, /k/, /i/
- Waulize wanafunzi sauti ipi wanayoisikia mwanzoni mwa kila neno lililofundishwa katika somo lililopita (**Usiandike Maneno**). [**maka, kima, ima, ama**]

Fundisha sauti **s** kwa kutumia muongozo ufuatao:

<p><b>Ujuzi</b></p> <p><b>Utambuzi wa Sauti</b></p> <p><b>(USIANDIKE)</b></p>	<p><b>Mwalimu “Ninatenda”</b></p> <p><i>Sauti mwanzo ya neno [saa] ni? /s/ Sikiliza, /sss/</i></p> <p><i>Sasa, sauti ya mwanzo ya neno [siki] ni? /s/ Sikiliza, /sss/</i></p>	<p><b>Mwalimu na Mwanafunzi “tunatenda”</b></p> <p><i>Rudia sauti zote na maneno</i></p> <p><i>Sasa, tuseme sauti ya mwanzo neno [saa]</i></p> <p><i>Kilammoja, sauti ya mwanzo ya neno [saa] ni /sss/</i></p> <p><i>Onesha ishara kwa mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja nawe (Haya sote tuseme) /sss/</i></p> <p><i>Sasa, fundisha sauti za mwanzo za neno [siki] kama ulivyofanya kwa [saa]</i></p>	<p><b>Mazoezi ya mwanafuzi “unatenda”</b></p> <p><b>Mwalimu aulize:</b> Ni sauti gani ya mwanzo mnayoisikia kwenye neno [saa/siki]?</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Mistari mitatu ya nyuma, sauti ipi?</b></li> </ul> <p><i>Wanafunzi watasema:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Mistari mitatu ya mbele, sauti ipi?</b></li> </ul> <p><i>Wanafunzi watasema:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Wasichana nyote, sauti ipi?</b></li> </ul> <p><i>Wanafunzi watasema:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Wavulana nyote, sauti ipi?</b></li> </ul> <p><i>Wanafunzi watasema:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Upande wangu wa kulia, sauti ipi?</b> (mwalimu aelekeze mkono upande wa kulia)</li> </ul> <p><i>Wanafunzi watasema:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Upande wangu wa kushoto, sauti ipi?</b></li> </ul>
---	---	---	---

			<p>(mwalimu aelekeze mkono upande wa kushoto)</p> <p>Wanafunzi watasema:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Nyote kwa pamoja, sauti ipi?</b></li> </ul> <p>Wanafunzi watasema:</p>
--	--	--	---

## Mazoezi ya utambuzi wa sauti

### Mchezo wa sauti:

- Waambie wanafunzi wainamishe vichwa vyao juu ya deski wakati wa mchezo huu wa sauti.
- Waambie wanafunzi waoneshe dole gumba juu wanaposikia sauti /s/ na dole gumba chini wasiposikia sauti hiyo mwanzoni mwa maneno yafuatayo: (USIYAANDIKE) [**saa, siki, sasa, saki, masa, kisa, masi, saka, sima**]

Maana yake “Ndiyo” Maana yake “hapana”

- Ita mwanafunzi mmoja mmoja aseme neno linaloanza na sauti /s/.
- Sahihisha makosa

## Maelekezo ya kufundisha utambuzi wa sauti ya herufi (Dakika 3-4)

### Marudio:

- Rudia herufi ulizofundisha: **a, m, k, i, s**
- Andika herufi ubaoni au tumia kadi za herufi. Waambie: **TIZAMA MAANDISHI.**
- Waoneshe wanafunzi kadi ya herufi **s** kisha waulize hiyo ni herufi gani
- Waulize wanafunzi kadhaa kuhakikisha kila mmoja amefahamu majina ya herufi.



Fundisha majina ya herufi **s** kutumia muongozo ufuatao.

<p><b>Msingi wa kialfabeti</b></p> <p><b>Uhusiano wa Sauti na herufi</b></p> <p><b>(ANDIKA)</b></p>	<p><b>Mwalimu:</b>  <b>“Ninatenda”</b>  <b>TIZAMA</b>  <b>MAANDISHI.</b></p> <p><i>Hii ni herufi s.</i>          Onesha wanafunzi herufi <b>s</b>. Herufi <b>s</b> inaunda sauti / <b>sss</b>/.</p>	<p><b>Mwalimu na mwanafunzi:</b>  <b>“Tunatenda”</b></p> <p><b>TIZAMA</b>  <b>MAANDISHI.</b></p> <p><i>Sasa, kila mmoja: Hii ni herufi s.</i> (Onesha wanafunzi herufi <b>s</b>) Herufi <b>s</b> inaunda sauti gani, sote kwa pamoja?          Onesha ishara kwa mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja nawe. (sote tuseme) /<b>sss</b>/</p>	<p><b>Mwalimu:</b>  <i>Sasa zamu yenu.</i>  <i>Darasa hii ni herufi?</i>          (Onesha herufi <b>s</b>)</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Mistari mitatu ya nyuma, sauti ipi?</b></li> </ul> <p><i>Wanafunzi watasema:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Mistari mitatu ya mbele, sauti ipi?</b></li> </ul> <p><i>Wanafunzi watasema:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Wasichana nyote, sauti ipi?</b> <i>Wanafunzi watasema:</i></li> <li>• <b>Wavulana nyote, sauti ipi?</b></li> </ul> <p><i>Wanafunzi watasema:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Upande wangu wa kulia, sauti ipi?</b> <i>(mwalimu aelekeze mkono upande wa kulia)</i></li> </ul> <p><i>Wanafunzi watasema:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Upande wangu wa kushoto, sauti ipi?</b> <i>(mwalimu aelekeze mkono upande wa kushoto)</i></li> </ul> <p><i>Wanafunzi watasema:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Nyote kwa pamoja, sauti ipi?</b></li> </ul> <p><i>Wanafunzi watasema:</i></p>
---	---	---	---

★ ★ **Mazoezi ya sauti ya herufi na ufasaha (4-5 dakika): MAZOEZI**

- Chukua kadi yenye herufi: **s** (AU andika herufi hiyo ubaoni).
- Wakumbushe wanafunzi jina la herufi kisha ioneshe huku ukiwataka wanyooshe mkono kama wanajua jina la herufi hiyo.

**(Tumia sekunde 30 au zaidi kwa kazi hii)**

- Tamka sauti ya herufi **s**
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono " kama wanaweza kutaja jina la herufi linalounda sauti hiyo.
- Waulize wanafunzi kama wanaweza kusoma neno kwa kulitamka. Onesha neno [**sima**] ubaoni kisha sema "**Tizama maandishi**".
- Waoneshe namna ya kutamka neno (**Ninatenda, Tunatenda, Unatenda**). /s/ /i/ /m/ /a/
- Uganisha sauti kisha sema neno [**sima**].
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kusema sauti zilizopo katika neno [**sima**], kisha watamke neno lote
- Chagua wanafunzi kadhaa kutamka neno hilo.
- Sahihisha makosa.
- Onesha neno kisha tamka sauti zinazounda neno
- Onesha neno kisha waambie wanafunzi walitamke. (**Mnatenda**).
- Onesha kila herufi kisha tamka pamoja na wanafunzi. Sauti ya mwanzo katika neno [**sima**] ni /sss/, inayofuata /iii/, inayofuata /mmm/, ya mwisho /aaa/. Neno gani hilo? [**sima**]. Neno hilo ni [**sima**].
- Sasa zamu yenu. Ni neno gani? [**sima**]
- Waambie wanafunzi waandike herufi mpya, silabi na maneno ambayo yamefundishwa katika kipindi hiki. (**Ninatenda, Tunatenda, Unatenda**)

**Sentensi rahisi:**

**Mama ana saa.**

**Mazoezi ya Kusoma Sentensi**

- Waoneshe wanafunzi kila herufi za sauti na utamke [**Mama ana saa.**]
- Waambie wanafunzi wasome sentensi **kwa sauti**

**Msamiati: (Dakika 4-5)**

RUDIA MANENO; [**siki, saa, sasa, sisi, ana, saka**]

**Rejea neno la hakiba:**

- Andika neno [**saa**] ubaoni.
- Wakumbushe wanafunzi kuwa neno hili limekwisha fundishwa.

Waambie walitumie katika sentensi kwa usahihi

Neno jipya [ana]:

- Waambie wanafunzi kuwa neno jipya lililotumiwa sana ni ana
- Waoneshe kadi ya neno au liandike ubaoni.
- Waambie wanafunzi wasome neno pamoja na wewe.

Mchezo wa kujenga ufasaha kutumia maneno; [saka, siki, sasa, sisi, ana]

- Waeleze wanafunzi wanyooshe mkono wanapoona neno wanalolitambua katika kadi utakayoonesha (au onesha maneno hayo ubaoni)
- Waambie kuwa utaonesha kila kadi (au utaonesha ubaoni) kwa haraka, kwa hiyo waharakishe kunyoosha mkono pindi wanapoona neno wanalolitambua
- Chagua mwanafunzi aliyenyoosha mkono asome neno husika.

**Ufahamu wa kusikiliza** (Dakika 10):

Wasomee hadithi ifuatayo. ANGALIZO: Msamiati na maneno rejea yamekozeshwa. Yaandike maneno ubaoni. Unapofikia msamiati wakati wa Mwanafunzi aweze kujibu maswali ya ufahamu , tulia kwa muda kisha onesha msamiati huo ubaoni.

**Ufahamu**

Sisi hapa ni watoto wadogo

Twajifunza kusoma na kuhesabu

Mwalimu wetu atufundisha adabu

Na heshima mbele ya wazazi wetu

**Maswali ya Ufahamu:**

- Watoto wadogo wanajifunza nini?
- Kwa nini tunajifunza kusoma na kuhesabu?
- Ni tabia gani nyengine njema mtoto anatakiwa kujifunza?

**Mazoezi:**

Waambie wanafunzi watafute maneno yanayoanza na sauti /s/

Weka alama ya **vyema** baada ya kufundisha

## 12.0 Kufundisha sauti S

### Wiki ya 3: Siku ya 2

<p>Tarehe: _____</p> <p><b>Muongozo wa ufundishaji:</b> Tumia <b>jina la herufi/sauti ya herufi</b> katika muongozo huu ili kufundisha majina na sauti za herufi husika</p> <p><b>Malengo:</b></p> <ul style="list-style-type: none"><li>• Mwanafunzi aweze kutamka sauti na jina la herufi sauti na jina la herufi <b>S</b> kwa kutumia muongozo ufuatao</li><li>• Mwanafunzi aweze kufanya mazoezi ya kusoma kwa kutumia kadi za herufi, maneno na sentensi</li><li>• Mwanafunzi aweze kusoma sentensi rahisi</li><li>• Mwanafunzi aweze kujibu maswali ya ufahamu</li></ul>	<p><b>Zana:</b></p> <ul style="list-style-type: none"><li>• Kadi za herufi <b>S</b></li><li>• Kadi za herufi kwa ajili ya marudio</li><li>• Kadi za maneno</li><li>• Andika neno [<b>Saa</b>] ubaoni</li><li>• Kadi za sentensi</li><li>• Hadithi au nyimbo</li><li>• Kitini cha mazoezi kwa mwanafunzi</li></ul>
--	---

### Muongozo wa kufundisha utambuzi wa sauti (Dakika 5)

#### Marudio:

- Rudia sauti zilizofundishwa katika wiki hiyo: /a/, /m/, /k/, /i/
- Waulize wanafunzi sauti ipi wanayoisikia mwanzoni mwa kila neno lililofundishwa katika somo lililopita (**Usiandike Maneno**). [**Maka, Kima, Ima, Ama**]

Fundisha sauti **S** kwa kutumia muongozo ufuatao:

<b>Ujuzi</b>	<b>Mwalimu "Ninatenda"</b>  <i>Sauti mwanzo ya neno [<b>Saa</b>] ni? /s/ Sikiliza, /s/</i>	<b>Mwalimu na Mwanafunzi "tunatenda"</b>  <i>Rudia sauti zote na maneno</i>  <i>Sasa, tuseme sauti ya mwanzo neno [<b>Saa</b>]</i>	<b>Mazoezi ya mwanafunzi "unatenda"</b>  <b>Mwalimu aulize:</b> Ni sauti gani ya mwanzo mnayoisikia kwenye neno [ <b>Saa/Siki</b> ]?
--------------	--	--	--

<p><b>Utambuzi wa Sauti</b></p> <p><b>(USIANDIKE)</b></p>	<p><i>Sasa, sauti ya mwanzo ya neno [Siki] ni? /s/ Sikiliza, /sss/</i></p>	<p><i>Kila mmoja, sauti ya mwanzo ya neno [Saa] ni /sss/ Onesha ishara kwa mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja nawe (Haya sote tuseme) /sss/</i></p> <p><i>Sasa, fundisha sauti za mwanzo za neno [Siki] kama ulivyofanya kwa [Saa]</i></p>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Mistari mitatu ya nyuma, sauti ipi?</b></li> </ul> <p><i>Wanafunzi watasema:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Mistari mitatu ya mbele, sauti ipi?</b></li> </ul> <p><i>Wanafunzi watasema:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Wasichana nyote, sauti ipi?</b></li> </ul> <p><i>Wanafunzi watasema:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Wavulana nyote, sauti ipi?</b></li> </ul> <p><i>Wanafunzi watasema:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Upande wangu wa kulia, sauti ipi?</b> (mwalimu aelekeze mkono upande wa kulia)</li> </ul> <p><i>Wanafunzi watasema:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Upande wangu wa kushoto, sauti ipi?</b> (mwalimu aelekeze mkono upande wa kushoto)</li> </ul> <p><i>Wanafunzi watasema:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Nyote kwa pamoja, sauti ipi?</b></li> </ul> <p><i>Wanafunzi watasema:</i></p>
---	--	---	--

## Mazoezi ya utambuzi wa sauti

### Mchezo wa sauti:

- Waambie wanafunzi wainamishe vichwa vyao juu ya deski wakati wa mchezo huu wa sauti.

- Waambie wanafunzi waoneshe dole gumba juu wanaposikia sauti /s/ na dole gumba chini wasiposikia sauti hiyo mwanzoni mwa maneno yafuatayo: (USIYAANDIKE) [saa, siki, sasa, saki, masa, kisa, masi, saka, sima]  
Maana yake “Ndiyo” Maana yake “hapana”
- Ita mwanafunzi mmoja mmoja aseme neno linaloanza na sauti /s/.
- Sahihisha makosa

## Maelekezo ya kufundisha utambuzi wa sauti ya herufi (Dakika 3-4)

### Marudio:

- Rudia herufi ulizofundisha: **A, M, K, I**
- Andika herufi ubaoni au tumia kadi za herufi. Waambie: **TIZAMA MAANDISHI.**
- Waoneshe wanafunzi kadi ya herufi **M** kisha waulize hiyo ni herufi gani
- Fanya hivyo kwa herufi **A, K, I**
- Waulize wanafunzi kadhaa kuhakikisha kila mmoja amefahamu majina ya herufi.

Fundisha majina ya herufi **S** kutumia muongozo ufuatao

<p><b>Msingi wa kialfabeti</b></p> <p><b>Uhusiano wa Sauti na herufi</b></p> <p><b>(ANDIKA)</b></p>	<p><b>Mwalimu:</b> “Ninatenda” <b>TIZAMA MAANDISHI.</b></p> <p><i>Hii ni herufi</i> <b>S.</b> Onesha wanafunzi herufi <b>S.</b> Herufi <b>S</b> inaunda sauti /sss/.</p>	<p><b>Mwalimu na mwanafunzi:</b> “Tunatenda”</p> <p><b>TIZAMA MAANDISHI.</b> <i>Sasa, kila mmoja:</i> <i>Hii ni herufi</i> <b>S.</b> (Onesha wanafunzi herufi <b>S</b>) Herufi <b>S</b> inaunda sauti gani, sote kwa pamoja? Onesha ishara kwa mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja nawe. (sote tuseme) / <b>sss/</b></p>	<p><b>Mwalimu:</b> <i>Sasa zamu yenu. Darasa hii ni herufi? (Onesha herufi S)</i></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Mistari mitatu ya nyuma, sauti ipi?</b> <i>Wanafunzi watasema:</i></li> <li>• <b>Mistari mitatu ya mbele, sauti ipi?</b></li> </ul>
---	--	--	---

			<p>Wanafunzi watasema:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Wasichana nyote, sauti ipi?</b> Wanafunzi watasema:</li> <li>• <b>Wavulana nyote, sauti ipi?</b></li> </ul> <p>Wanafunzi watasema:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Upande wangu wa kulia, sauti ipi?</b> (mwalimu aelekeze mkono upande wa kulia)</li> </ul> <p>Wanafunzi watasema:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Upande wangu wa kushoto, sauti ipi?</b> (mwalimu aelekeze mkono upande wa kushoto)</li> </ul> <p>Wanafunzi watasema:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Nyote kwa pamoja, sauti ipi?</b></li> </ul> <p>Wanafunzi watasema:</p>
--	--	--	--

★ ★ **Mazoezi ya sauti ya herufi na ufasaha (4-5 dakika): MAZOEZI**

- Chukua kadi yenye herufi: **S** (AU andika herufi hiyo ubaoni).
- Wakumbushe wanafunzi jina la herufi kisha ioneshe huku ukiwataka wanyooshe mkono kama wanajua jina la herufi hiyo.

**(Tumia sekunde 30 au zaidi kwa kazi hii)**

- Tamka sauti ya herufi **S**
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono " " kama wanaweza kutaja jina la herufi linalounda sauti hiyo.
- Waulize wanafunzi kama wanaweza kusoma neno kwa kulitamka. Onesha neno **[sima]** ubaoni kisha sema "**Tizama maandishi**".
- Waoneshe namna ya kutamka neno (**Ninatenda, Tunatenda, Unatenda**). /s/ /i/ /m/ /a/

- Unganisha sauti kisha sema neno **[Sima]**.
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kusema sauti zilizopo katika neno **[Sima]**, kisha watamke neno lote.
- Chagua wanafunzi kadhaa kutamka neno hilo.
- Sahihisha makosa.
- Onesha neno kisha tamka sauti zinazounda neno
- Onesha neno kisha tamka sauti zinazounda neno
- Onesha neno kisha waambie wanafunzi walitamke. (**Mnatenda**).
- Onesha kila herufi kisha tamka pamoja na wanafunzi. Sauti ya mwanzo katika neno **[Sima]** ni /sss/, inayofuata /iii/, inayofuata /mmm/, ya mwisho /aaa/. Neno gani hilo? **[sima]**. Neno hilo ni **[Sima]**.
- Waambie wanafunzi waandike herufi mpya, silabi na maneno ambayo yamefundishwa katika kipindi hiki. (**Ninatenda, Tunatenda, Unatenda**)

### Sentensi rahisi:

**Mama ana saa.**

### Mazoezi ya Kusoma Sentensi

- Waoneshe wanafunzi kila herufi za sauti na utamke **[Mama ana saa.]**
- Waambie wanafunzi wasome sentensi **kwa sauti**

### Msamiati: (Dakika 4-5)

RUDIA MANENO; **[Siki, Saa, Sasa, Sisi, Ana, Saka]**

### Rejea neno la hakiba:

- Andika neno **[Saa]** ubaoni.
- Wakumbushe wanafunzi kuwa neno hili limekwisha fundishwa. Waambie walitumie katika sentensi kwa usahihi

### Neno jipya **[ana]**:

- Waambie wanafunzi kuwa neno jipya lililotumiwa sana ni **ana**
- Waoneshe kadi ya neno au liandike ubaoni.
- Waambie wanafunzi wasome neno pamoja na wewe.

### Mchezo wa kujenga ufasaha kutumia maneno; **[Saka, Siki, Sasa, Sisi, ana]**

- Waeleze wanafunzi wanyooshe mkono wanapoonana neno wanalolitambua katika kadi utakayoonesha (au onesha maneno hayo ubaoni)
- Waambie kuwa utaonesha kila kadi (au utaonesha ubaoni) kwa haraka,



kwa hiyo waharakishe kunyoosha mkono pindi wanapooa neno wanalolitambua

- Chagua mwanafunzi aliyenyoosha mkono asome neno husika.

**Ufahamu wa kusikiliza** (Dakika 10):

Wasomee hadithi ifuatayo. ANGALIZO: Msamiati na maneno rejea yamekozesha na yamepigwiwa mstari. Yaandike maneno ubaoni. Unapofikia msamiati wakati wa Mwanafunzi aweze kujibu maswali ya ufahamu , tulia kwa muda kisha oneshwa msamiati huo ubaoni.

**Ufahamu:**

Sisi hapa ni watoto wadogo  
Twajifunza kusoma na kuhesabu  
Mwalimu wetu atufundisha adabu  
Na heshima mbele ya wazazi wetu

**Maswali ya Ufahamu:**

- Watoto wadogo wanajifunza nini?
- Kwa nini tunajifunza kusoma na kuhesabu?
- Ni tabia gani nyengine njema mtoto anatakiwa kujifunza?

**Mazoezi:** Waambie wanafunzi watafute maneno yanayoanza na sauti /s/

Weka alama ya **vyema** baada ya kufundisha

### 13.0 Kufundisha sauti o

#### Wiki ya 3: Siku ya 3

<p>Tarehe: _____</p> <p><b>Muongozo wa ufundishaji:</b> Tumia <b>jina la herufi/sauti ya herufi</b> katika muongozo huu ili kufundisha majina na sauti za herufi husika</p> <p><b>Malengo:</b></p> <ul style="list-style-type: none"><li>• Mwanafunzi aweze kutamka sauti na jina la herufi sauti na jina la herufi <b>o</b> kwa kutumia muongozo ufuatao</li><li>• Mwanafunzi aweze kufanya mazoezi ya kusoma kwa kutumia kadi za herufi, maneno na sentensi</li><li>• Mwanafunzi aweze kusoma sentensi rahisi</li><li>• Mwanafunzi aweze kujibu maswali ya ufahamu</li></ul>	<p><b>Zana:</b></p> <ul style="list-style-type: none"><li>• Kadi za herufi <b>o</b></li><li>• Kadi za herufi kwa ajili ya marudio</li><li>• Kadi za maneno</li><li>• Andika neno [<b>omo</b>] ubaoni</li><li>• Kadi za sentensi</li><li>• Hadithi au nyimbo</li><li>• Kitini cha mazoezi kwa mwanafunzi</li></ul>
--	---

#### Muongozo wa kufundisha utambuzi wa sauti (Dakika 5)

##### Marudio:

- Rudia sauti zilizofundishwa katika wiki hiyo: /a/, /m/, /k/, /i/, /s/
- Waulize wanafunzi sauti ipi wanayoisikia mwanzoni mwa kila neno lililofundishwa katika somo lililopita (**Usiandike Maneno**). [**maka, kima, ima, ama, siki, saa, kisa**]

Fundisha sauti **o** kwa kutumia muongozo ufuatao:

Ujuzi	Mwalimu "Ninatenda"	Mwalimu na Mwanafunzi "tunatenda" <i>Rudia sauti zote na maneno</i>	Mazoezi ya mwanafuzi "unatenda"

<p><b>Utambuzi wa Sauti</b></p> <p><b>(USIANDIKE)</b></p>	<p>Sauti mwanzo ya neno <b>[oa]</b> ni? /o/ Sikiliza, /ooo/</p> <p>Sasa, sauti ya mwanzo ya neno <b>[omo]</b> ni? /o/ Sikiliza, /ooo/</p>	<p>Sasa, tuseme sauti ya mwanzo neno <b>[oa]</b>  <i>Kilammoja, sauti ya mwanzo ya neno [oa] ni /ooo/</i>  <i>Onesha ishara kwa mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja nawe (Haya sote tuseme) /ooo/</i></p> <p>Sasa, fundisha sauti za mwanzo za neno <b>[omo]</b> kama ulivyofanya kwa <b>[oa]</b></p>	<p><b>Mwalimu aulize:</b> Ni sauti gani ya mwanzo mnayoisikia kwenye neno <b>[oa/omo]</b>?</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Mistari mitatu ya nyuma, sauti ipi?</b></li> </ul> <p>Wanafunzi watasema:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Mistari mitatu ya mbele, sauti ipi?</b></li> </ul> <p>Wanafunzi watasema:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Wasichana nyote, sauti ipi?</b></li> </ul> <p>Wanafunzi watasema:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Wavulana nyote, sauti ipi?</b></li> </ul> <p>Wanafunzi watasema:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Upande wangu wa kulia, sauti ipi?</b> (mwalimu aelekeze mkono upande wa kulia)</li> </ul> <p>Wanafunzi watasema:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Upande wangu wa kushoto, sauti ipi?</b> (mwalimu aelekeze mkono upande wa kushoto)</li> </ul> <p>Wanafunzi watasema:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Nyote kwa pamoja, sauti ipi?</b></li> </ul> <p>Wanafunzi watasema:</p>
---	---	---	--

## Mazoezi ya utambuzi wa sauti

### Mchezo wa sauti:

- Waambie wanafunzi wainamishe vichwa vyao juu ya deski wakati wa mchezo huu wa sauti.
- Waambie wanafunzi waoneshe dole gumba juu wanaposikia sauti /o/ na dole gumba chini wasipoisikia sauti hiyo mwanzoni mwa maneno yafuatayo: (USIYAANDIKE) [**oa, omo, oka, soma, somo, kimo, simo, ona**] Maana yake "Ndiyo" Maana yake "hapana"
- Ita mwanafunzi mmoja mmoja aseme neno linaloanza na sauti /o/.
- Sahihisha makosa

### Maelekezo ya kufundisha utambuzi wa sauti ya herufi (Dakika 3-4)

#### Marudio:

- Rudia herufi ulizofundisha: **a, m, k, i, s, o**
- Andika herufi ubaoni au tumia kadi za herufi. Waambie: **TIZAMA MAANDISHI.**
- Waoneshe wanafunzi kadi ya herufi **o** kisha waulize hiyo ni herufi gani
- Fanya hivyo kwa herufi **a, m, i, s, k**
- Waulize wanafunzi kadhaa kuhakikisha kila mmoja amefahamu majina ya herufi.

Fundisha majina ya herufi **o** kutumia muongozo ufuatao

<b>Msingi wa kialfabeti</b>  <b>Uhusiano wa Sauti na herufi (ANDIKA)</b>	<b>Mwalimu: "Ninatenda"</b> <b>TIZAMA MAANDISHI.</b>  <i>Hii ni herufi</i> <b>o.</b> Onesha wanafunzi herufi <b>o.</b> Herufi <b>o</b> inaunda sauti / <b>ooo/.</b>	<b>Mwalimu na mwanafunzi: "Tunatenda"</b>  <b>TIZAMA MAANDISHI.</b> <i>Sasa, kila mmoja:</i> <i>Hii ni herufi</i> <b>o.</b> (Onesha wanafunzi herufi <b>o</b> ) Herufi <b>o</b> inaunda sauti gani, sote kwa pamoja?	<b>Mwalimu:</b> <i>Sasa zamu yenu.</i> <i>Darasa hii ni herufi?</i> (Onesha herufi <b>o</b> ) <ul style="list-style-type: none"><li>• <b>Mistari mitatu ya nyuma, sauti ipi?</b></li></ul> <i>Wanafunzi watasema:</i> <ul style="list-style-type: none"><li>• <b>Mistari mitatu ya mbele, sauti ipi?</b></li></ul> <i>Wanafunzi watasema:</i> <ul style="list-style-type: none"><li>• <b>Wasichana nyote, sauti ipi?</b></li></ul> <i>Wanafunzi watasema:</i>
--	---	---	--

		<p>Onesha ishara kwa mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja nawe. (sote tuseme) /ooo/</p>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Wavulana nyote, sauti ipi?</b> Wanafunzi watasema:</li> <li>• <b>Upande wangu wa kulia, sauti ipi?</b> (mwalimu aelekeze mkono upande wa kulia) Wanafunzi watasema:</li> <li>• <b>Upande wangu wa kushoto, sauti ipi?</b> (mwalimu aelekeze mkono upande wa kushoto) Wanafunzi watasema:</li> <li>• <b>Nyote kwa pamoja, sauti ipi?</b> Wanafunzi watasema:</li> </ul>
--	--	--	--

★ ★ **Mazoezi ya sauti ya herufi na ufasaha (4-5 dakika): MAZOEZI**

- Chukua kadi zenye herufi: **o** (AU andika herufi hiyo ubaoni).
- Wakumbushe wanafunzi jina la herufi kisha ioneshe huku ukiwataka wanyooshe mkono kama wanajua jina la herufi hiyo.

**(Tumia sekunde 30 au zaidi kwa kazi hii)**

- Tamka sauti ya herufi **o**
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kutaja jina la herufi linalounda sauti hiyo.
- Waulize wanafunzi kama wanaweza kusoma neno kwa kulitamka. Onesha neno **[omo]** ubaoni kisha sema “**Tizama maandishi**”.
- Waoneshe namnaya kutamka neno (**Ninatenda, Tunatenda, Unatenda**).  
**/o/ /m/ /o/**
- Uganisha sauti kisha sema neno **[omo]**.
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kusema sauti

- zilizopo katika neno **[omo]**, kisha watamke neno lote
- Chagua wanafunzi kadhaa kutamka neno hilo.
  - Sahihisha makosa.
  - Onesha neno kisha tamka sauti zinazounda neno
  - Onesha neno kisha waambie wanafunzi walitamke. (**Mnatenda**).
  - Onesha kila herufi kisha tamka pamoja na wanafunzi. Sauti ya mwanzo katika neno **[omo]** ni **/ooo/**, inayofuata **/mmm/**, ya mwisho **/ooo/**. Neno gani hilo? **[omo]**. Neno hilo ni **[omo]**.
  - Sasa zamu yenu. Ni neno gani? **[omo]**
  - Waambie wanafunzi waandike herufi mpya, silabi na maneno ambayo yamefundishwa katika kipindi hiki. (**Ninatenda, Tunatenda, Unatenda**)

### Sentensi rahisi:

#### Mama ana omo

- Waoneshe wanafunzi kila herufi za sauti na utamke **[mama ana omo]**
- Waambie wanafunzi wasome sentensi **kwa sauti**

### Msamiati: (Dakika 4-5)

RUDIA MANENO;

#### Rejea neno la hakiba:

- Andika neno **[omo]** ubaoni.
- Wakumbushe wanafunzi kuwa neno hili limekwisha fundishwa. Waambie walitumie katika sentensi kwa usahihi

#### Neno jipya: [ana]

- Waambie wanafunzi kuwa neno jipya lililotumiwa sana ni
- Waoneshe kadi ya neno au liandike ubaoni.
- Waambie wanafunzi wasome neno pamoja na wewe.

#### Mchezo wa kujenga ufasaha kutumia maneno; **[oa, omo, oka, oga, ona, ota]**

- Waelezew wanafunzi wanyooshemkonowanapoonaneno wanalolitambua katika kadi utakayoonesha (au onesha maneno hayo ubaoni)
- Waambie kuwa utaonesha kila kadi (au utaonesha ubaoni) kwa haraka, kwa hiyo waharakishe kunyoosha mkono pindi wanapoonaneno wanalolitambua
- Chagua mwanafunzi aliyenyoosha mkono asome neno husika.

## Ufahamu wa kusikiliza (Dakika 10):

Wasomee hadithi ifuatayo. ANGALIZO: Msamiati na maneno rejea yamekozesha na yamepigwiwa mstari. Yaandike maneno ubaoni. Unapofikia msamiati wakati wa Mwanafunzi aweze kujibu maswali ya ufahamu, tulia kwa muda kisha oneshwa msamiati huo ubaoni.

## Ufahamu:

Siku moja mama alikwenda sokoni kununua sabuni omo afulie nguo. Aliipenda sana maana inafanya nguo ziwe safi. Omo ni nzuri kwa kufulia. Sabuni ya Omo inaondoa madoa yote ya uchafu katika nguo. Ukitumia omo huwezi kuona uchafu tena katika nguo.

## Mazoezi:

Waambie wanafunzi watafute maneno yanayoanza na sauti /o/

Weka alama ya **vyema** baada ya kufundisha

## 14.0 Kufundisha sauti O

### Wiki ya 3: Siku ya 4

<p>Tarehe: _____</p> <p><b>Muongozo wa ufundishaji:</b> Tumia <b>jina la herufi/sauti ya herufi</b> katika muongozo huu ili kufundisha majina na sauti za herufi husika</p> <p><b>Malengo:</b></p> <ul style="list-style-type: none"><li>• Mwanafunzi aweze kutamka sauti na jina la herufi sauti na jina la herufi <b>O</b> kwa kutumia muongozo ufuatao</li><li>• Mwanafunzi aweze kufanya mazoezi ya kusoma kwa kutumia kadi za herufi, maneno na sentensi</li><li>• Mwanafunzi aweze kusoma sentensi rahisi</li><li>• Mwanafunzi aweze kujibu maswali ya ufahamu</li></ul>	<p><b>Zana:</b></p> <ul style="list-style-type: none"><li>• Kadi za herufi <b>O</b></li><li>• Kadi za herufi kwa ajili ya marudio</li><li>• Kadi za maneno</li><li>• Andika neno [<b>Omo</b>] ubaoni</li><li>• Kadi za sentensi</li><li>• Hadithi au nyimbo</li><li>• Kitini cha mazoezi kwa mwanafunzi</li></ul>
--	---

## Muongozo wa kufundisha utambuzi wa sauti (Dakika 5)

### Marudio:

- Rudia sauti zilizofundishwa katika wiki hiyo: /a/, /m/, /k/, /i/, /s/
- Waulize wanafunzi sauti ipi wanayoisikia mwanzoni mwa kila neno lililofundishwa katika somo lililopita (**Usiandike Maneno**). [*maka, kima, ima, ama, siki, saa, kisa*]

Fundisha sauti **O** kwa kutumia muongozo ufuatao:

Ujuzi	Mwalimu "Ninatenda"	Mwalimu na Mwanafunzi "tunatenda"	Mazoezi ya mwanafunzi "unatenda"
Utambuzi wa Sauti	<i>Sauti mwanzo ya neno [Oa] ni? /o/ Sikiliza, /ooo/</i>	<i>Rudia sauti zote na maneno</i>	<b>Mwalimu aulize:</b> Ni sauti gani ya mwanzo mnayoisikia kwenye neno [Oa/Omo]? <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Mistari mitatu ya nyuma, sauti ipi?</b></li> </ul>
(USIANDIKE)	<i>Sasa, sauti ya mwanzo ya neno [Omo] ni? /o/ Sikiliza, /ooo/</i>	<i>Sasa, tuseme sauti ya mwanzo neno [Oa]</i> <i>Kilammoja, sauti ya mwanzo ya neno [Oa] ni /ooo/</i> <i>Onesha ishara kwa mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja nawe (Haya sote tuseme) /ooo/</i>	<i>Wanafunzi watasema:</i> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Mistari mitatu ya mbele, sauti ipi?</b></li> </ul> <i>Wanafunzi watasema:</i> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Wasichana nyote, sauti ipi?</b></li> </ul> <i>Wanafunzi watasema:</i> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Wavulana nyote, sauti ipi?</b></li> </ul> <i>Wanafunzi watasema:</i> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Upande wangu wa kulia, sauti ipi?</b> (mwalimu aelekeze mkono upande wa kulia)</li> </ul>
		<i>Sasa, fundisha sauti za mwanzo za neno [Omo] kama ulivyofanya kwa [Oa]</i>	



			<p>Wanafunzi watasema:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Upande wangu wa kushoto, sauti ipi?</b> (mwalimu aelekeze mkono upande wa kushoto)</li> </ul> <p>Wanafunzi watasema:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Nyote kwa pamoja, sauti ipi?</b></li> </ul> <p>Wanafunzi watasema:</p>
--	--	--	--

## Mazoezi ya utambuzi wa sauti

### Mchezo wa sauti:

- Waambie wanafunzi wainamishe vichwa vyao juu ya deski wakati wa mchezo huu wa sauti.
- Waambie wanafunzi waoneshe dole gumba juu wanaposikia sauti /o/ na dole gumba chini wasiposikia sauti hiyo mwanzoni mwa maneno yafuatayo: (USIYAANDIKE) [**Aa, Omo, Oka, Soma, Somo, Kimo, Simo, Ona**] Maana yake “Ndiyo” Maana yake “hapana”
- Ita mwanafunzi mmoja mmoja aseme neno linaloanza na sauti /o/.
- Sahihisha makosa

## Maelekezo ya kufundisha utambuzi wa sauti ya herufi (Dakika 3-4)

### Marudio:

- Rudia herufi ulizofundisha: **A, M, K, I, S, O**
- Andika herufi ubaoni au tumia kadi za herufi. Waambie: **TIZAMA MAANDISHI.**
- Waoneshe wanafunzi kadi ya herufi **K** kisha waulize hiyo ni herufi gani
- Fanya hivyo kwa herufi **A, M, I, S, O**
- Waulize wanafunzi kadhaa kuhakikisha kila mmoja amefahamu majina ya herufi.

Fundisha majina ya herufi **O** kutumia muongozo ufuatao

<p><b>Msingi wa kialfabeti</b></p> <p><b>Uhusiano wa Sauti na herufi</b></p> <p><b>(ANDIKA)</b></p>	<p><b>Mwalimu: “Ninatenda”</b></p> <p><b>TIZAMA MAANDISHI.</b></p> <p><i>Hii ni herufi</i></p> <p><b>O.</b> Onesha wanafunzi herufi</p> <p><b>O.</b> Herufi <b>O</b> inaunda sauti / <b>ooo/</b>.</p>	<p><b>Mwalimu na mwanafunzi: “Tunatenda”</b></p> <p><b>TIZAMA MAANDISHI.</b></p> <p><i>Sasa, kila mmoja: Hii ni herufi</i></p> <p><b>O.</b> (Onesha wanafunzi herufi <b>O</b>) Herufi <b>O</b> inaunda sauti gani, sote kwa pamoja?</p> <p>Onesha ishara kwa mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja nawe. (sote tuseme) /<b>ooo/</b></p>	<p><b>Mwalimu:</b></p> <p><i>Sasa zamu yenu. Darasa hii ni herufi? (Onesha herufi <b>O</b>)</i></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Mistari mitatu ya nyuma, sauti ipi?</b></li> </ul> <p><i>Wanafunzi watasema:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Mistari mitatu ya mbele, sauti ipi?</b></li> </ul> <p><i>Wanafunzi watasema:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Wasichana nyote, sauti ipi?</b> Wanafunzi watasema:</li> <li>• <b>Wavulana nyote, sauti ipi?</b></li> </ul> <p><i>Wanafunzi watasema:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Upande wangu wa kulia, sauti ipi?</b> (mwalimu aelekeze mkono upande wa kulia)</li> </ul> <p><i>Wanafunzi watasema:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Upande wangu wa kushoto, sauti ipi?</b> (mwalimu aelekeze mkono upande wa kushoto)</li> </ul> <p><i>Wanafunzi watasema:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Nyote kwa pamoja, sauti ipi?</b></li> </ul> <p><i>Wanafunzi watasema:</i></p>
---	---	---	---

## ★ ★ Mazoezi ya sauti ya herufi na ufasaha (4-5 dakika): MAZOEZI

- Chukua kadi yenye herufi: **O** (AU andika herufi hiyo ubaoni).
- Wakumbushe wanafunzi jina la herufi kisha ioneshe huku ukiwataka wanyooshe mkono kama wanajua jina la herufi hilo.

### (Tumia sekunde 30 au zaidi kwa kazi hii)

- Tamka sauti ya herufi **O**
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kutaja jina la herufi linalounda sauti hiyo.
- Waulize wanafunzi kama wanaweza kusoma neno kwa kulitamka. Onesha neno **[Omo]** ubaoni kisha sema “**Tizama maandishi**”.
- Waoneshe namna ya kutamka neno (**Ninatenda, Tunatenda, Unatenda**).  
**/o/ /m/ /o/**
- Unganisha sauti kisha sema neno **[Omo]**.
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kusema sauti zilizopo katika neno **[Omo]**, kisha watamke neno lote.
- Chagua wanafunzi kadhaa kutamka neno hilo.
- Sahihisha makosa.
- Onesha neno kisha tamka sauti zinazounda neno
- Onesha neno kisha waambie wanafunzi walitamke. (**Mnatenda**).
- Onesha kila herufi kisha tamka pamoja na wanafunzi. Sauti ya mwanzo katika neno **[Omo]** ni **/ooo/**, inayofuata **/mmm/**, ya mwisho **/ooo/**. Neno gani hilo? **[Omo]**. Neno hilo ni **[Omo]**.
- Sasa zamu yenu. Ni neno gani? **[Omo]**
- Waambie wanafunzi waandike herufi mpya, silabi na maneno ambayo yamefundishwa katika kipindi hiki. (**Ninatenda, Tunatenda, Unatenda**)

### Sentensi rahisi:

**Mama ana omo**

### Mazoezi ya Kusoma Sentensi

- Waoneshe wanafunzi kila herufi za sauti na utamke **[Mama ana omo]**
- Waambie wanafunzi wasome sentensi kwa sauti

## **Msamiati: (Dakika 4-5)**

RUDIA MANENO;

### **Rejea neno la hakiba:**

- Andika neno [**Omo**] ubaoni.
- Wakumbushe wanafunzi kuwa neno hili limekwisha fundishwa. Waambie walitumie katika sentensi kwa usahihi

### **Neno jipya:**

- Waambie wanafunzi kuwa neno jipya lililotumiwa sana ni
- Waoneshe kadi ya neno au liandike ubaoni.
- Waambie **wanafunzi** wasome neno pamoja na wewe.

### **Mchezo wa kujenga ufasaha** kutumia maneno; [**Oa, Ona, Omo, Kosa, Soma, Soka, Kimo, Mosi**]

- Waeleze wanafunzi wanyooshe mkono wanapona neno wanalolitambua katika kadi utakayoonesha (au onesha maneno hayo ubaoni)
- Waambie kuwa utaonesha kila kadi (au utaonesha ubaoni) kwa haraka, kwa hiyo waharakishe kunyoosha mkono pindi wanapona neno wanalolitambua
- Chagua mwanafunzi aliyenyoosha mkono asome neno husika.

### **Ufahamu wa kusikiliza** (Dakika 10):

Wasomee hadithi ifuatayo. ANGALIZO: Msamiati na maneno rejea yamekozeshwa na yamepigiwa mstari. Yaandike maneno ubaoni. Unapofikia msamiati wakati wa Mwanafunzi aweze kujibu maswali ya ufahamu , tulia kwa muda kisha onesha msamiati huo ubaoni.

### **Ufahamu:**

Siku moja mama alikwenda sokoni kununua sabuni ya omo afulie nguo. Aliipenda sana maana inafanya nguo ziwe safi. Omo ni nzuri kwa kufulia. Omo inaondoa madoa yote ya uchafu katika nguo. Ukitumia omo huwezi kuona uchafu tena katika nguo.

### **Maswali ya ufahamu:**

- Mama alikwenda wapi?
- Omo hutusaidia kufanya nini?
- Nyumbani mnamtia sabuni gani kufulia?

## Mazoezi:

Waambie wanafunzi watafute maneno yanayoanza na sauti /o/

Weka alama ya **vyema** baada ya kufundisha

## 15.0 Marudio ya herufi kubwa na ndogo

### Wiki ya 3: Siku ya 5

<p>Tarehe: _____</p> <p><b>Muongozo wa ufundishaji:</b> Tumia <b>jina la herufi/sauti ya herufi</b> katika muongozo huu ili kufundisha herufi na sauti za herufi husika</p> <p><b>Malengo:</b></p> <ul style="list-style-type: none"><li>• Rudia sauti ya herufi na jina la <b>sS, oO</b></li><li>• Kutumia maelekezo ya hapo chini</li><li>• Fanya mazoezi kwa kutumia kadi za herufi</li><li>• Soma sentensi zilizorahisi</li><li>• Soma hadithi</li></ul>	<p><b>Zana:</b></p> <ul style="list-style-type: none"><li>• Kadi za herufi <b>sS, oO</b></li><li>• Kadi za herufi kwa ajili ya marudio</li><li>• Kadi za maneno</li><li>• Andika neno [<b>sima</b>] ubaoni</li><li>• Kadi za sentensi</li><li>• Hadithi au Nyimbo</li><li>• Kitini cha mazoezi kwa wanafunzi</li></ul>
--	--

### Muongozo wa kufundisha Utambuzi wa Sauti (Dakika 5)

#### ★ Marudio:

- Rudia sauti zilizofundishwa katika wiki hiyo: /s/, /o/
- Waulize wanafunzi sauti ipi wanayoisikia mwanzoni mwa kila neno lililofundishwa katika somo lililopita (**Usiandike Maneno**).

Rudia sauti kwa kutumia muongozo ufuatao.

<b>Ujuzi</b>	<b>Mwalimu</b> "Ninatenda"	<b>Mwalimu na mwanafunzi</b> "Tunatenda" <i>Rudia sauti zote za maneno</i>	<b>Mazoezi ya mwanafunzi</b> "Unatenda"
--------------	-------------------------------	--	--

<p><b>Utambuzi wa Sauti</b></p> <p><b>(USIANDIKE)</b></p>	<p>Mwalimu aongoze kutambua sauti za mwanzo za maneno tofauti kutoka masomo yaliyotangulia.</p>	<p>Sasa, Tuseme sauti ya mwanzo kutoka katika maneno tofauti tuliyojifunza somo lililopita.</p>	<p><b>Mwalimu anasema:</b> Ni sauti ipi ya mwanzo mnayosikia (Rejea maneno ya masomo yaliyopita)</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Mistari mitatu ya nyuma, ni sauti ipi?</b></li> </ul> <p>Wanafunzi watasema:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Mistari mitatu ya mbele, ni sauti ipi?</b></li> </ul> <p>Wanafunzi watasema:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Wasichana nyote, ni sauti ipi?</b></li> </ul> <p>Wanafunzi watasema:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Wavulana nyote, ni sauti ipi?</b></li> </ul> <p>Wanafunzi watasema:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Upande wangu wa kulia, sauti ipi?</b> (Mwalimu aelekeze mkono upande wa kulia)</li> </ul> <p>Wanafunzi watasema:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Upande wangu wa kushoto, sauti ipi?</b> (Mwalimu aelekeze mkono wa kushoto)</li> </ul> <p>Wanafunzi watasema:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Nyote kwa pamoja, sauti ipi?</b></li> </ul> <p>Wanafunzi watasema:</p>
---	---	---	---

## Mazoezi ya Utambuzi wa Sauti

### Mchezo wa Sauti:

- Waambie wanafunzi wasimame wanaposikia sauti ya mwanzo ya maneno waliyojifunza (USIYAANDIKE)
- Sahihisha makosa

### Maelekezo ya kufundisha utambuzi wa sauti ya herufi (Dakika 3-4)

#### Marudio:

- Rudia herufi ulizofundishwa ambazo ni **sS, oO**
- Andika herufi ubaoni au tumia kadi za herufi. Waambie: **TIZAMA MAANDISHI.**
- Waulize wanafunzi ni herufi gani na waioneshe **sS, oO**
- Waulize wanafunzi kadhaa kuhakikisha kila mmoja amefahamu majina ya herufi.
- Chagua herufi kutoka katika masomo yaliyopita ili wanafunzi wayafanyie mazoezi

Rudia majina ya herufi **sS, oO** kutumia muongozo ufuatao.

Msingi wa kialfabeti	Mwalimu: "Ninatenda"	Mwalimu na mwanafunzi: "Tunatenda"	Mwanafunzi: "Unatenda"
Uhusiano wa Sauti na herufi (ANDIKA)	<b>TIZAMA MAANDISHI.</b> <i>Hii ni herufi sS.</i> Onesha wanafunzi <b>sS</b> . Herufi <b>sS</b> inatoa sauti /sss/.  <i>Hii ni herufi oO.</i> (Onesha wanafunzi <b>oO</b> ). Herufi <b>oO</b> inatoa sauti /ooo/.	<b>TIZAMA MAANDISHI.</b> <i>Kila mmoja: Hii ni sauti sS.</i> (Onesha wanafunzi <b>sS</b> ). <i>Sauti sS inatoa sauti gani, kila mmoja?</i> Nyoosha mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja na wewe. (darasa zima) / <b>sss</b> /	Mwalimu wagawie wanafunzi kadi za maneno katika makundi na waambie wachague herufi zinaashiria sauti zilizotamkwa

		<p>Sasa Kila mmoja:  Hii ni herufi  <b>oO</b>. (Onesha  wanafunzi herufi  <b>oO</b>) Herufi <b>oO</b>  inaunda sauti  gani, kila mmoja?  Nyoosha mkono  kuashiria  wanafunzi wajibu  pamoja na wewe.  (Darasa zima) /  <b>ooo/</b></p>	
--	--	--	--

★ ★ **Mazoezi ya Sauti ya herufi na Ufasaha (Dakika 4-5): MAZOEZI**

- Chukua kadi zenye herufi **sS, oO** (AU andika herufi hizo ubaoni).
- Wakumbushe wanafunzi jina la kila herufi kisha onesha moja baada ya nyingine huku ukiwataka wanyooshe mkono kama wanajua majina ya herufi hizo.

**(Tumia sekunde 30 au zinazokaribiana kwa zoezi hili)**

- Sema sauti ya herufi **sS**
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kusema jina la herufi linalounda sauti hiyo. Fanya hivyo kwa **oO**.
- Waulize wanafunzi kama wanaweza kusoma neno kwa kulitamka. Onesha neno; **[takata, utamu, peleka]** kwenye ubao na useme **“Tizama Maandishi”**.
- Waoneshe namna ya kutamka neno (**Ninatenda, Tunatenda, Unatenda**) **/s/ /i/ /m/ /a/**
- Unganisha sauti kisha sema neno **[sima]**. Fanya hivyo kwa neno **[omo]**
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kusema sauti zilizomo katika neno **[Sima]**, na kisha watamke neno lote **[Sima]**
- Chagua wanafunzi kadhaa kutamka neno hiyo.
- Sahihisha makosa.
- Onesha neno kisha tamka sauti zinazounda neno
- Onesha neno kisha waambie wanafunzi walitamke. **[Mnatenda]**.



- Onesha kila herufi kasha tamka pamoja na wanafunzi. auti ya mwanzo katika neno **[sima]** ni /sss/, inayofuata /iii/ inayofuata /mmm/, ya mwisho /aaaa/. Ni neno gani hilo? **[sima]**. Neno ni **[sima]**.
- Sasa zamu yenu. Neno gani? **[sima]**
- Waambie wanafunzi waandike herufi mpya, silabi na maneno ambayo yamefundishwa katika kipindi hicho (**Ninatenda, Tunatenda, Unatenda**)

### **Mchezo wa kujenga ufasaha** kutumia maneno **[saa, sima, saka, oa, omo, ona]**

- Waeleze wanafunzi wanyooshe mkono wanpoona neno wanalolitambua katika kadi utakayoonyesha (au onesha maneno hayo ubaoni).
- Waambie kuwa utaonesha kila kadi (au utaonesha ubaoni) kwa haraka, kwa hiyo waharakishe kunyoosha mkono pindi wanapoona neno wanalolitambua
- Chagua mwanafunzi aliyenyoosha mkono asome neno husika.

### **Msamiati: (Dakika 4-5)**

Rudia maneno **[saa, sima, saka, oa, omo, ona]**

### **Ufahamu wa Kusikiliza** (Dakika 10):

Wasomee hadithi ifuatayo. ANGALIZO: Msamiati na maneno rejea yamekozeshwa na yamepigwiwa mstari. Yaandike maneno ubaoni. Unapofikia msamiati wakati wa Mwanafunzi aweze kujibu maswali ya ufahamu, tulia kwa muda kisha onesha msamiati huo ubaoni.

### **Hadithi ya Kusoma kwa Sauti [Hadithi kutoka kwenye kitabu]**

- Andika hadithi kutoka kwenye kitabu ubaoni.
- Andika jina la mwandishi wa hadithi ubaoni
- Andika jina la msanifu wa michoro ubaoni.

### **Rejea neno la hakiba:**

- Andika neno **[sima]** ubaoni.
- Wakumbushe wanafunzi kuwa neno hili limekwisha fundishwa.
- Waambie walitumie katika sentensi kwa usahihi

Weka alama ya **vyema** baada ya kufundisha

## 16.0 Marudio na kutilia mkazo (Chagua herufi kutoka siku tofauti)

### Wiki ya 4: Siku ya 1

<p>Tarehe: _____</p> <p><b>Muongozo wa ufundishaji:</b> Tumia <b>jina la herufi/sauti ya herufi</b> katika muongozo huu ili kufundisha majina na sauti za herufi husika</p> <p><b>Malengo:</b></p> <ul style="list-style-type: none"><li>• Mwanafunzi aweze kutamka sauti na jina la herufi sauti na jina la herufi <b>m, i</b> kwa kutumia muongozo ufuatao</li><li>• Mwanafunzi aweze kufanya mazoezi ya kusoma kwa kutumia kadi za herufi, maneno na sentensi</li><li>• Mwanafunzi aweze kusoma sentensi rahisi</li><li>• Mwanafunzi aweze kujibu maswali ya ufahamu</li></ul>	<p><b>Zana:</b></p> <ul style="list-style-type: none"><li>• Kadi za herufi <b>m, i</b></li><li>• Kadi za herufi kwa ajili ya marudio</li><li>• Kadi za maneno</li><li>• Andika neno [<b>mama</b>] ubaoni</li><li>• Kadi za sentensi</li><li>• Hadithi au nyimbo</li><li>• Kitini cha mazoezi kwa wanafunzi</li></ul>
---	--

### Muongozo wa kufundisha utambuzi wa sauti (Dakika 5)

#### ★ Marudio:

- Rudia sauti zilizofundishwa mwezi huu: /m/, /i/
- Waulize wanafunzi sauti ipi wanaisikia mwanzoni mwa kila neno lililofundishwa katika somo lililopita (**USIANDIKE maneno**).

Rudia sauti kwa kutumia muongozo ufuatao:

<b>Ujuzi</b>	<b>Mwalimu "Ninatenda"</b>	<b>Mwalimu na mwanafunzi "tunatenda"</b> <i>Rudia sauti zote na maneno</i>	<b>Mazoezi ya mwanafunzi "unatenda"</b>
--------------	--------------------------------	---	---

